




Nina marafiki wengi.




Baadhi ya marafiki zangu wana umri mkubwa kuniliko na...



Baadhi yao ni wadogo kuliniko.



Baadhi ya marafiki zangu ni wakongwe.



Na baadhi yao ni wadogo sana!



Baadhi ya marafiki zangu wako na mikia...



Baadhi ya marafiki zangu hawana miguu.




Baadhi ya marafiki zangu huruka. Baadhi yao wanaogelea.






Oh! Vitabu ni rafiki yangu sana!



Lakini ni nani rafiki yangu zaidi?



Mama yangu!!!

